**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**
***(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)***
**S.L.P 4 NZEGA - MKOA WA TABORA**
Simu: 026 269 2349 Nukushi: md@nzegadc.go.tz
Fax: 026 269 2349 Tovuti: www.nzegadc.go.tz

---

**Unapojibu tafadhali taja:**
Kumb. Na. NDC/L1/4/Vol.I/47

23 Januari, 2026

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA ZA WAKUSANYA MAPATO (REVENUE COLLECTORS)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega anakaribisha maombi kwa watanzania wenye sifa za kujaza nafasi kumi na saba (17) za kazi ya mkataba kwa Wakusanya Mapato ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

### 1.0 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukusanya mapato ya Halmashauri katika kituo cha kazi utakachopangiwa.
ii. Kukagua na kuhakikisha kila mzigo unaopita katika kituo chako umelipiwa ushuru, na kukatiwa risiti.
iii. Ukaguzi wa nyaraka za kusafirishia mizigo ili kuona kama ni halali au zimegushiwa.
iv. Kumtoza faini mtu yoyote atakayekutwa na hatia ikiwa ni ya kugushi nyaraka au kusafirisha mzigo bila kulipia au bila kibali cha kusafirishia mizigo hiyo, faini hiyo itazingatia muongozo wa sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.
v. Kutunza POS (Point of Sell) ziwe katika hali ya usalama.
vi. Kulinda mapato ya Halmashauri yasitoroshwe.
vii. Kulinda mali zote za Halmashauri ya Wilaya.
viii. Pamoja na majukumu mengine yote utakayopangiwa na mwajiri wako.

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI ZA WAKUSANYA MAPATO

i. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne (IV), Mwenyewe sifa zaidi itakuwa vizuri zaidi.
ii. Awe na uwezo wa kutumia vifaa vya kidigitali.
iii. Awe tayari kufanya kazi kwenye kituo chochote atakachopangiwa.
iv. Awe na hali njema ya kiafya itakayomruhusu kutimiza majukumu yake bila changamoto yoyote.

**1.2 MASHARTI KWA WAOMBAJI**

i. Mwombaji anatakiwa awe ni raia wa Tanzania mwenye umri si chini ya miaka 18 na usiozidi 45
ii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma ambavyo ni vyeti vya kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho pamoja na vyeti vya kuhitimu mafunzo mabalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
iii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingeleza
iv. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **13 Februari, 2026** saa tisa na nusu jioni.

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha Barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Aidha, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nzega,
S. L. P 4,
**NZEGA – TABORA**

Imetolewa na;

Mohamed O. Sume
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**NZEGA**